
# MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA, 2022) KWA MAENEO YA KASKAZINI MWA MKOA WA KIGOMA

**Umetolewa: (02/09/2022)**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa msimu wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba - Disemba, 2022; athari na ushauri kwa sekta mbalimbali kaskazini mwa mkoa wa Kigoma na wilaya zake:

(I) Ngazi ya Mkoa




Kielelezo 1: (a) Mwelekeo wa msimu wa Vuli, 2022 katika maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Kigoma. (b) Ramani inayoonesha wastani wa muda mrefu wa mvua za msimu wa Vuli katika sehemu mbalimbali katika maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Kigoma. **Angalizo**: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za mwezi Oktoba hadi Disemba, mabadiliko ya mvua kati ya mwaka mmoja na mwingine yamezingatiwa.

**Dondoo**

- *Kwa ujumla mvua za Chini ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya kaskazini mwa mkoa wa Kigoma.*
- *Mvua zinatarajiwa kuanza katika wiki ya nne ya Septemba, 2022.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha Januari, 2023.*
- *Vipindi virefu vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi vinatarajiwa katika msimu huu wa Vuli.*

**Mvua za msimu wa Vuli, 2022**

Kwa ujumla mvua zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi ya kaskazini mwa mkoa wa Kigoma. Msimu unatarajiwa kuanza kwa kusuasua na kuambatana na vipindi virefu vya ukavu.


***Angalizo:***

*Ingawa maeneo mengi yanatarajiwa kupata mvua za chini ya wastani hadi wastani, izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza yakajitokeza katika maeneo machache.*

(II) Ngazi ya Wilaya

## MWELEKEO WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA, 2022) KWA WILAYA YA KAKONKO
## Umetolewa: 02/09/2022

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba-Disemba, 2022; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Kakonko, Kigoma.




Mwelekeo wa mvua za Vuli (Oktoba-Disemba, 2022) kwa wilaya ya Kakonko, Kigoma.

### Dondoo muhimu

- *Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Kakonko.*
- *Mvua zitaanza wiki ya nne ya Septemba, 2022 na zinatarajiwa kuanza kwa kusuasua kutokana na kuwepo vipindi virefu vya ukavu.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha Januari, 2023.*
- *Wakulima na wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji na uzalishaji wa mazao ili kukabiliana na upungufu wa mvua.*

### Mvua za msimu wa Vuli, 2022 kwa wilaya ya Kakonko

**Zitaanza:** Wiki ya nne ya Septemba, 2022.

**Zitaisha:** Januari, 2023.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa chini ya wastani hadi wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Oktoba-Disemba kwa wilaya ya Kakonko ni kati ya milimita 370 hadi 380.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Disemba, 2022.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano mkubwa wa kutokea vipindi virefu vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Vuli, 2022.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache na zenye mtawanyiko hafifu katika maeneo mengi ukilinganisha na Vuli iliyopita.

### Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**
- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

**Matokeo**

- Upungufu wa unyevunyevu katika udongo katika maeneo mengi unaweza kuathiri uzalishaji wa mazao.
- Upungufu wa mvua unaweza kuathiri upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo.


**Ushauri**

- Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora za muda mfupi zinazoendana na urefu wa msimu.
- Wakulima wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua.
- Wafugaji wanashauriwa kufuata njia bora za ufugaji ikiwemo kupanda malisho na uhifadhi.

(II) Ngazi ya Wilaya

## MWELEKEO WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA, 2022) KWA WILAYA YA KIBONDO, KIGOMA
## Umetolewa: 02/09/2022

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba-Disemba, 2022; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Kibondo, Kigoma.




Mwelekeo wa mvua za Vuli (Oktoba-Disemba, 2022) kwa wilaya ya Kibondo, Kigoma

### Dondoo muhimu

- *Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Kibondo.*
- *Mvua zitaanza wiki ya nne ya Septemba, 2022 na zinatarajiwa kuanza kwa kusuasua kutokana na kuwepo vipindi virefu vya ukavu.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha Januari, 2023.*
- *Wakulima na wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji na uzalishaji wa mazao ili kukabiliana na upungufu wa mvua.*

### Mvua za msimu wa Vuli, 2022 kwa wilaya ya Kibondo

**Zitaanza:** Wiki ya nne ya Septemba, 2022.

**Zitaisha:** Januari, 2023.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa chini ya wastani hadi wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Oktoba-Disemba kwa wilaya ya Kibondo ni kati ya 360 hadi 380.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Disemba, 2022.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano mkubwa wa kutokea vipindi virefu vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Vuli, 2022.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache na zenye mtawanyiko hafifu katika maeneo mengi ukilinganisha na Vuli iliyopita.

### Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**
- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

#### Matokeo

- Upungufu wa unyevunyevu katika udongo katika maeneo mengi unaweza kuathiri uzalishaji wa mazao.
- Upungufu wa mvua unaweza kuathiri upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo.

#### Ushauri

- Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora za muda mfupi zinazoendana na urefu wa msimu.
- Wakulima wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua.
- Wakulima wanashauriwa kutumia mbinu bora zinazohifadhi unyevunyevu katika udongo.
- Wafugaji wanashauriwa kufuata njia bora za ufugaji ikiwemo kupanda malisho na uhifadhi.